

14. HEART OF DARKNESS

14. HEART OF DARKNESS

Karibu kwenye muhtasari wa kitabu cha KUMI NA NNE kwenye orodha ya vitabu 100 ninavyosoma kwa siku 100.

HEART OF DARKNESS ni riwaya iliyoandikwa na JOSEPH CONRAD inayohusu simulizi ya safari ya kuelekea katikati ya pori kubwa kumuokoa mtu aliyekwama huko.



Marlow, mkurugenzi wa makampuni, mwanasheria na mhasibu wako kwenye boti kubwa na ya kifahari baharini.

Ni katikati ya bahari na giza ni nene. Mkurugenzi ndiye nahodha wa boti hiyo.

Marlow ni bahari mzoefu, ambaye amekuwa kwenye kila aina ya meli na kila aina ya bahari. Kwake kila meli na kila bahari ni kitu kile kile.

Marlow anawaeleza wenzake jinsi eneo walipo sasa lilivyo eneo la giza na kuwaambia kutafuta ufanisi ndiyo kumeokoa nchi zao.

Anaeleza jinsi ukoloni ulivyotokana na kutafuta ufanisi zaidi. Pale rasilimali kwenye nchi husika zilipotumika kwa kiwango cha juu, walienda nchi nyingine kuwapora rasilimali zao.

Anawaeleza ushindi wa wakoloni haukutokana na uimara wao, bali walitumia udhaifu wa wale waliowatawala.

Mto Thames wa London una mafuriko, hivyo wapo baharini kusubiri mpaka mafuriko hayo yaishe.

Marlow anaelezea jinsi alivyoingia kwenye ubaharia. Anawaambia tangu akiwa mtoto alipenda kuangalia ramani ya dunia na kujiambia nikiwa mkubwa nitatembelea hapa.

Aliona mto mmoja mtefu sana na ukamvutia, akajiambia lazima atembelee mto huo kwa wakati huo.

Akawa anauliza kila mtu amsaidie lakini hakupata msaada, ila hakukata tamaa. Aliendelea kutafuta kila fursa na baadaye akasikia kuna kapteni ambaye ameuawa kwenye mto huo, kulitokea kutokuelewana na wenyeji katika kuuziana kuku wawili, akaanza kumpiga kiongozi wa eneo hilo na ndipo akauawa.

Baada ya kumuua kampteni, watu wa eneo lile walikimbia kabisa kwa kuwa walijua wenzake na kapteni watakuja kulipa kisasi.

Hivyo alipata fursa ya kwenda kuchukua nafasi iliyoachwa na kapteni aliyeuawa, alifika na kukuta mabaki ya mwili wake yako pale alipouawa.

Alienda kwenye ofisi za kampuni atakayofanyia kazi na kupokelewa vizuri, anatambulishwa kwa watu mbalimbali, anapewa fomu za kuweka sahihi na kutakiwa kwenda kwa daktari kupimwa.

Kampuni anayoenda kufanyia kazi ni ya wafaransa, yeye ni muingezera na eneo walipo ni la watu weusi.

Wakati daktari anachukua maelezo yake, anamtahadharisha kwamba huko anakoenda anatakiwa awe mtulivu sana, wengi wanaoenda huwa hawarudi.

Marlow anaanza kupata wasiwasi, maisha ya huko yakoje.

Anapewa maelekezo ya kuelekea eneo lake la kazi, ambapo atakuwa anaendeaha boti kwenye mto huo mrefu.

Wanasafiri kwa siku 30 mpaka kufika kituo chake cha kazi, njiani wanapishana na watu weusi wengi, wengi wao wakiwa uchi na wakiendelea na maisha yao kama kawaida.

Katika mazungumzo na nahodha wa boti waliyokuwa wanatumia, Marlow anaendelea kujifunza kwamba watu wengi wanaoenda huko huwa hawarudi wakiwa hai, anamweleza kuhusu mmoja aliyejinyonga, alipouliza kwa nini akajibiwa hakuna anayejua.

Akiwa amefika kwenye kituo chake cha kazi anaona kundi la watu weusi waliofungwa kwa mnyororo shingoni, afya zao ni dhoofu. Anajiambia kwa hali walizonazo watu hao, hawawezi kuwa na uhalifu ambao wanatuhumiwa kuwa nao.

Anazunguka kwenye eneo hilo na kukuta kundi la watu wengine weusi wamekaa chini ya miti, afya zao ni dhoofu sana. Hao wameshafanyishwa sana kazi kiasi kwamba hawawezi tena, hivyo wanaachiwa huru waende wakajifie.

Marlow anampa mmoja biskuti aliyokuwa nayo, anaichukua haraka na kuila, anaonekana kuwa na njaa kali.

Marlow anaona jinsi ambavyo watu hao wanateswa, huku wakiwa hawana hatia yoyote.

Anakutana na mtu mweupe kwenye stesheni hiyo, ambaye ni mhasibu wa kampuni hiyo, anamuona akiwa kwenye hali nzuri.

Anasuburi hapo kwenye stesheni kwa siku kumi kabla ya kwenda ndani zaidi kutekeleza majukumu yake. Mhasibu yule anakuwa naye karibu na kumweleza atakapoenda ndani zaidi atakutana na Kurtz ambaye ndiye mkuu wa stesheni hiyo na huwa ni mtu mwenye bidii kwenye kazi zake. Anamweleza jinsi Kurtz atakavyofika mbali kwenye kampuni hiyo kwa namna anavyojituma sana.

Wakiwa hapo kwenye stesheni anaona watu weusi wengi ambao afya zao ni mbovu na wenye njaa, wengine wakiwa wanakufa kwa magonjwa na njaa

Marlow akiongozana na kundi la watu 60 wanaanza safari ya kuelekea ndani zaidi kwenye mto huo mrefu ambapo ndipo boti lake lilipo.

Safari ni ya maili 200 ambazo wanapita porini na hali ya hewa siyo nzuri. Siku ya 15 wanafika kwenye mto na kukuta kituo kingine. Wanapokelewa na anajitambulisha, anaambiwa boti anayopaswa kutumia imezama hivyo inapaswa kutolewa kwenye maji na kufanyiwa matengenezo.

Marlow anajiuliza atakuwa anafanya nini kwenye mazingira hayo kwa siku ambazo boti inatengenezwa.

Marlow anakutana na meneja wa kituo hicho, mtu mweupe pekee ambaye amekaa eneo hilo kwa muda mrefu, wengine wote huwa wanaishia kufa au kushindwa na kuondoka.

Anamuona siyo mtu mwenye akili au uwezo sana, hivyo atakuwa amepewa umeneja huo kwa kuwa ana uzoefu wa muda mrefu na kwa kuwa hali ya hewa haijamkataa kama wengine.

Meneja anamueleza Marlow kwamba anapaswa kuanza kazi mara moja kwani kuna vituo ambavyo hali zake siyo nzuri, moja wapo kiliwa kituo cha Kurtz.

Marlow anamwambia kwamba amesikia Kurtz akuzungumziwa kwenye kituo kikuu, anamwambia ni mmoja wa watu wanaofanya vizuri sana, ila kwa sasa ana wasiwasi kituo chake kinaweza kuwa kwenye hali mbaya, kwani kwa muda mrefu hakuna boti imeenda huko.

Siku iliyofuata Marlow alianza kazi ya matengenezo ya boti, ghafla akaona moto mkubwa unaunguza shamba. Aliona watu wakikimbia na baadaye mtu mweusi akipigwa sana kwamba ndiye amesababisha moto huo.

Baadaye alimuona meneja akiwa na mtu mwingine, meneja anamwambia matukio ya aina hiyo yapo. Anaondoka na kumwacha Marlow na yule mtu mwingine, ambaye anajifunza kwamba amekuwa hapo zaidi ya mwaka, kazi aliyoletwa kufanya ni kutengeneza matofali lakini hajaanza kwa sababu kuna vitu havipo.

Marlow anajifunza sehemu kubwa ya watu walio kwenye kituo hicho hakuna kazi wanazofanya, kuna vitu wanasubiri ndiyo majukumu yao yaanze.

Mtu yule anamweleza kuhush Kurtz, jinsi alivyo mtu wa kutegemewa na pia anamwambia amesikia waliomleta Kurtz ndiyo pia waliomleta yeye Marlow.

Anaendelea kumwambia miaka miwili ijayo Krantz atakuwa mbali sana kwenye kampuni hiyo.

Mtu yule anaonekana kama anamuonea Marlow wivu kwa kuwa atakuwa karibu zaidi na Kurtz.

Kwa kuwa watu wengi pale hawana majukumu ya kazi, wamekuwa wanatumia muda wao kuhangaika na mambo ya wengine.

Marlow anaendelea kutengeneza boti atakalolitumia kwenye kazi yake, lakini kuna vifaa anavyohitaji na inabidi vikachukuliwe mbali.

Inaonekana hakuna anayejali sana kuhusu vifaa hivyo au boti kuwa tayari mapema hivyo inabidi ashinikize sana kupatikana kwa vifaa hivyo kwa kuwa Krantz anahitaji kufikiwa.

Anaahidiwa ndani ya wiki tatu vifaa vitakuwa vimepatikana, lakini kinachotokea kwenye wiki hizo tatu

ni kituo chao kinavamiwa na wakoloni wengine ambao wao wanachojali ni kupata pembe za ndovu na mali zaidi kutoka eneo hilo.



Kiongozi wa kundi lililovamia kituo ambacho Marlow alikuwepo ni mjomba wa meneja wa kituo hicho, hivyo mara zote wanaonekana wakiwa pamoja.

Siku moja Marlow akiwa kwenye boti anawasikia wakisemezana kuhusu Kurtz, ambaye alikuja na mzigo mkubwa wa pembe za ndovu ila labla hajafika kwenye kituo akarudi alikotoka, huku akiwaacha wasaidizi wake ndiyo wafikishe mzigo.

Mjomba anasikika akimwambia meneja kwamba hali ya hewa itamsaidia kukamilisha lengo lake. Inaonekana wanachotaka ni Kurtz afe maana ndiyo kikwazo kwao.

Marlow aliwasikiliza wakiongea kwa muda mrefu, meneja akieleza jinsi hali ya hewa imemkubali na wote wanaokuja wanakufa na kumuacha.

Siku chache baadaye kundi lililowavamia linaondoka kwenda ndani zaidi.

Matengenezo ya boti yanakamilika na Marlow anaanza safari yake ya kwanza kuelekea ndani zaidi kwenye eneo hilo. Kwenye safari hiyo ameambatana na meneja wa kituo na watu wengine.

Safari inaendelea, ni safari ngumu kuliko Marlow alivyodhani.

Kwanza inachukua muda mrefu, kwa zaidi ya siku mbili wako kwenye maji, usiku na mchana huku hatari ikiwa ni kubwa.

Pili hawakubeba chakula cha kutosha, hivyo njaa iliwasumbua sana.

Tatu hali ya hewa haikuwa nzuri, siku ya tatu walikutana na ukungu mkubwa ambapo hawakuweza hata kuona mbele.

Nne walivamiwa na kushambuliwa kwa mishale, kitu kilichopelekea mmoja wa wasaidizi wa kuendesha boti kufariki dunia.

Muda wote Marlow alikuwa anahofia kwamba Kurtz atakuwa kwenye hatari na hatapata nafasi ya kuongea naye. Kwa yale aliyosikia kuhusu Kurtz, alitamani sana akutane naye na kuongea naye.

Pamoja na ugumu wa safari wanafanikiwa kumrikiya Kurtz na matatu makubwa yanamshangaza Marlow,

Jambo la kwanza ni hali ya afya ya Kurtz, siyo nzuri, amedhoofu lakini bado anaonekana kuwa na matumaini makubwa.

Jambo la pili ni kiwango kikubwa cha pembe za ndovu ambazo Kurtz alikuwa amekusanya, Marlow anajiambia hadhani kama kuna pembe ya ndovu iliyokuwa imesalia eneo hilo.

Jambo la tatu ni jinsi Kurtz alivyokuwa anaita kila kitu ni chake, anasema mto wangu, msitu wangu, pembe zangu za ndovu. Kila kitu alikiita chake, jambo lililomshangaza Marlow kwa umiliki huo Kurtz aliojipa.

Anashangazwa pia na jinsi kitu pekee ambacho Kurtz alikuwa anafikiria ni pembe za ndovu, anaona anaichukulia dunia kama sehemu ya kusimama ili kukamilisha matakwa yake, tofauti na wengine wanaoichukulia dunia kama mahali pa kuishi na hivyo kujali mambo mengine yanayoendelea.



Marlow anakutana na mtu ambaye amekuwa na Kurtz kwa muda mrefu na kumweleza jinsi anavyomjua Kurtz.

Kwanza anamwambia jinsi ambavyo walijikuta wanasogea na kuzidi kuingia ndani na ndani zaidi. Kila wakati walijiambia wanaenda na watarudi, lakini walijikuta hawarudi.

Lakini pia anaeleza jinsi Kurtz alivyoweza kupata kiwango kikubwa cha pembe za ndovu kutoka kwa wenyeji bila hata ya kuwa na vitu vya kubadilishana nao, alikuwa na ushawishi mkubwa kwa watu hao.

Anaeleza jinsi siku moja Kurtz alitaka kumuua kwa sababu alimkuta akiwa na pembe za ndovu alizopewa kama zawadi na wenyeji. Kurtz alimtaka ampe pembe hizo la sivyo atamuua, na alijua hatanii, hivyo ilibidi ampe.

Pia anaeleza jinsi alivyomuuguza Kurtz alipoumwa sana mara mbili, mara zote Kurtz akiahidi kuondoka, lakini akipona anarudi porini kutafuta pembe za ndovu.

Marlow anamuuliza kuhusu mafuvu ya vichwa vya watu ambayo yamewekwa chini ya dirisha anamjibu walikuwa waasi ambao waliuawa.

Marlow anashangazwa waasi wa aina gani, anamjibu kuishi maisha kama ya Kurtz ni kazi kubwa, kwa sababu unatengeneza maadui wengi.

Anamuuliza kama yeye hana maadui, anamjibu yeye ni mtu wa kawaida, hana mawazo makuu, hakuna kikubwa anachotaka kwa wengine hivyo hakuna anayeweza kuwa anataka kumuua.

Licha ya kuwa hoi kitandani, bado Kurtz alikuwa anawataka waliomzunguka wamtibu ili arudi kwenda kukusanya pembe za ndovu.

Alipomuona Marlow alionekana kufurahi na kusema afadhali amefika, Marlow anajiambia kwamba atakuwa alikuwa anatumiwa barua kuambiwa anakuja.

Meneja anamueleza Marlow kwamba kwa Kurtz hakuna tena wanachoweza kufanya kumsaidia, wameshafanya kila wanaloweza lakini hali yake ni mbaya.

Anamweleza japo Kurtz aliweza kupata pembe nyingi za ndovu, njia alizotumia siyo sahihi na hilo litaleta hasara kubwa kwenye kampuni.

Marlow anamjibu pamoja na hayo bado anaona Kurtz alikuwa mtu mzuri, Meneja anakasirishwa na kusikia hilo na kuondoka.

Marlow anamwambia yule aliyekuwa na Kurtz atafute namna na kuondoka maana kubaki hapo ni hatari kwake, meneja hatamuacha salama.

Mtu huyo anamjibu ana marafiki wengi kwa wenyeji na ataenda huko, anamtaka Marlow alinde heshima ya Kurtz.

Kabla hajaondoka anamueleza Marlow kwamba Kurtz hakutaka kabisa kuondoka, hata boti yao ilipokaribia, aliamrisha ishambuliwe ili wasimfikie.

Kurtz anatoroka, Marlow anamtafuta na kukuta ameshafika mbali, anaelekea kwenye msitu mkubwa akiwa anatambaa.

Anamtaka arudi maana ni hatari kwake, Kurtz anamwambia amuache, kwa sababu ana mipango mikubwa na yuko salama.

Anamshawishi mpaka wanarudi na wanaanza safari ya kurudi kwenye kituo kikuu.

Meneja na wenzake wanamchukulia Kurtz ni kama ameshakufa na Marlow wamemuweka kwenye kundi moja na Kurtz.

Wakiwa safarini Kurtz anatoa karatasi zilizoandikwa na kumpa Marlow akimwambia hana imani na meneja.

Safari inasimama kwa muda kwa ajili ya matengenezo ya boti, Kurtz anafariki dunia na kuzikwa.

Marlow anaona kwa nini aliamini Kurtz alikuwa mtu mzuri na alisimama upande wake mpaka mwisho.

Pamoja na madhaifu yake, Kurtz alikuwa mtu ambaye alisema na kusimamia alichuamini bila kuyumbishwa. Na mpaka mauti yanamfika, hakuwa amekata tamaa, bado aliamini anakwenda kufanya makubwa.

Marlow anarudi mjini akiwa na mawazo mengi na kila alipoona watu aliwaona kama ni usumbufu kwake.

Aliwachukulia kwa dharau akiona hawawezi kujua yale anayojua yeye, wengi walidhani anaumwa na hivyo kujaribu jitihada mbalimbali za kumsaidia.

Karatasi za maandiko mbalimbali ambazo Kurtz alimuachia, bado anazo na hajachunguza sana kilicho ndani.

Mwakilishi wa kampuni anamtafuta na kutaka ampe maandiko ya Kurtz kwa sababu ni mali ya kampuni. Marlow anamwambia ni maandiko binafsi, mwakilishi huyo anasisitiza apewe.

Marlow anampa sehemu ya maandiko hayo, anayapitia na kuona hayana manufaa kwa kampuni.

Binamu wa Kurtz pia anamtafuta, anamweleza jinsi alivyokuwa mwanamuziki mzuri, Marlow anazidi kushangazwa na uwezo mkubwa aliokuwa nao Kurtz.

Mwandishi wa habari pia anamtafuta na kumwambia japo Kurtz hakuwa mwandishi mzuri, alikuwa mnenaji bora na mwenye ushawishi mkubwa. Anamwambia kama Kurtz angeingia kwenye siasa, angefika mbali zaidi.

Marlow anamkabidhi baadhi ya maandiko ya Kurtz na mwandishi huyo anasema atayachapa.

Marlow anabaki na barua binafsi alizoandika Kurtz na picha ya mwanamke aliyoichora.

Marlow anapanga kupeleka barua na picha hiyo kwa mhusika, kwa kuwa Kurtz alimwamini na kumuachia.

Anakumbuka kabla Kurtz hajafa alimwambia pembe za ndovu zilizopo amezipata kwa juhudi zake mwenyewe na siyo mali ya kampuni. Ila anajua kampuni itasema ni mali yake, kitu ambacho hawezi kukizuia, ila siyo haki.

Marlow anaenda kwa mwanamke yule na kupokelewa, anamkuta bado yuko kwenye majonzi, japo ni mwaka tangu Kurtz afariki dunia.

Mwanamke huyo anamueleza jinsi alivyompenda na kumwamini Kurtz, jinsi alivyokuwa kila kitu kwake na jinsi alivyompa furaha. Sasa maisha yake yamebaki kuwa huzuni, na mbaya zaidi amefia mbali.

Marlow anamueleza jinsi Kurtz alivyomfia, jinsi naye alivyomuelewa na kumkubali na jinsi atakavyomkumbuka milele.

Wanasikitika kwa pamoja pale, mwanamke yule anamwambia ni wao wawili tu walioweza kumwelewa Kurtz, jinsi alivyokuwa mtu mwema na mkuu, ambaye wengi hawakumuelewa.

Kurtz alikuwa na mahusiano na mwanamke huyo kwa muda mrefu, ila hawakuwa wameoana kwa sababu ndugu wa mwanamke hawakumkubali Kurtz, huenda kwa kuwa hakuwa tajiri. Na hilo ndiyo lililomsukuma Kurtz kwenda kupambana mwenyewe ili kujijengea utajiri na kuyapoteza maisha yake katika mpango huo.

Mwanamke yule anamtaka amwambia maneno ya mwisho aliyosema Kurtz kabla hajafa, Marlow anamjibu alitaja jina lake. Mwanamke huyo anafurahi na kusema alijua hilo kabisa, japo ndani yake Marlow anajiambia neno lake la mwisho lilikuwa ni kutaka haki.

Marlow anamalizia simulizi hiyo na kukaa kimya akifanya tahajudi, huku waliokuwa wanamsikiliza nao pia wakikaa kimya.

👉SOMO

Riwaya hii ni ya kipekee kwenye mfuatano wa visa mbalimbali, lakini imebeba ujumbe mkubwa kuhusu maisha, hasa mapambano ya kufanikiwa.

Tumeona jinsi ambavyo Kurtz ana msukumo mkubwa wa kufanikiwa na haoni kingine chochote ila mafanikio yake. Hata dakika za mwisho, bado anawaza mafanikio yake.

Pia tumeona nguvu ya mapenzi katika kumpa msukumo mkubwa mtu. Mtu anapopenda kweli, huwa tayari kufanya chochote kwa ajili ya mapenzi yake.

Tumeona pia jinsi ukoloni na unyonyaji ulivyo na madhara kwa wenyeji wanaonyonywa, wanateswa na kufanyishwa kazi mpaka kufa. Na wale wanaokataa mateso hayo wanauawa kama maadui au waasi.

Tumejifunza pia jinsi mfumo wa urasimu unavyopunguza ufanisi, kwa kutoa mwanya wa watu kuwa bila kazi kwa sababu kuna vitu wanasubiri. Serikali na taasisi nyingi kubwa huendeshwa kwa urasimu, hivyo kuwa na wafanyakazi wengi ambao hawana uzalishaji wowote.

Pamoja na kiu kubwa ya mafanikio unayoweza kuwa nayo, hupaswi kusahau au kupuuza maeneo mengine muhimu kwenye maisha yako na hata ya wengine pia. Usichukue kwa wengine na kuwaumiza kwa manufaa yako.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,

www.t.me/somavitabutanania